**KANISA NA UAMSHO**

Na Mchg. Dkt. Faith Lugazia

Awali ya yote namshukuru Mungu wa Utatu aliyenitia nguvu na kuniwezesha kusimama mbele yenu wajoli wenzangu. Pili ninaishukuru Halmashauri Kuu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) iliyopitisha jina langu na kuniomba nishirikiane nanyi katika mada hii: "Kanisa na Uamsho." Kipekee ninajiona kuheshimiwa sana kuwa na maongezi na waheshimiwa wastahiki kama ninyi ambao ni manabii mnaolipa maono Kanisa la kesho na kujua kesho ya kanisa.

Ninyi ni watendakazi, nikitumia msemo wa Dkt. Jesse Mugambi: 'Ninyi ni manabii mlioitwa kutuliza wale wanaosumbuliwa na kusumbua wale waliotulia pasipokujali gharama zitakazowakuta ili Kristo ahubiriwe.' Ushiriki wenu katika Missioni ya Mungu umefanya KKKT kuwa Kanisa la mfano wa kuigwa duniani. Si tu kwa Walutheri bali madhehebu mengine pia yanayokiri kuwa Yesu Kristo ni Mwokozi wa Ulimwengu na vyote vilivyomo. Niungane na Mtume Paulo kuwapongeza: "Endeleeni kuimarika wala msitikisike kwa kuwa taabu yenu si bure katika Bwana" (1Kor.15:58-59).

Nimepewa mada isemayo "Kanisa na Uamsho" Niseme tangu mwanzo kuwa habari ya Kanisa na uamsho si ngeni kihistoria. Uinjlisti na uamsho ndani ya Kanisa vimekwenda bega kwa bega katika uhai wa kanisa lote duniani. Kibiblia tunaona tangu mwanzo mara baada ya Kanisa kuzaliwa, ukristo haukuruhusiwa na utawala wa Kirumi uliokuwepo, wote tunafahamu kuuawa kwa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo moja ya sababu ni kutokana na suala la kisiasa. Kulikuwa na sababu za kiimani kwamba mara baada ya Ukristo kuruhusiwa, dini ya himaya ya Kirumi, tatizo kubwa hasa lilihusu ufahamu wa watu kuhusu Yesu Kristo wakijiuliza kuwa atarudi ili aweze kutuondoa katika mateso haya ya duniani na je ni Mungu ama mwanadamu, Roho Mtakatifu ni nani na Mungu Baba, mwana na Roho Mtakatifu wanafanya kazi vipi na hawa wanahusianaje na kutofautianaje katika Utendaji (Makundi mbali mbali ndani ya Kanisa yalitoa mawazo yao). Hebu nitaje kwa kifupi makundi sita na jinsi walivyoona wao.

1.**Montana** waliotoa Unabii kuwa Kristo anarudi karibuni kwa hiyo watu sasa wawe na maadili mema na kukaza sana juu ya matendo na kwa kiasi kikubwa kusahau Imani.[1]

2.**Wa Mornakia**-waliokazania umoja wa Mungu kiasi cha kukataa uanadamu wa Yesu Kristo na kuwa Kristo na Roho Mtakatifu wana nafasi moja tu na si sehemu ya utatu.[2]

3. **Macedonius** walisema: "Roho Mtakatifu si sehemu ya Utatu Mtakatifu wa Mungu. Roho ni kiumbe tu na ni mmoja ya Roho zinazohudumu na malaika lakini kwa kiasi anatofautiana na malaika. Na wakaongeza kuwa kama Roho Mtakatifu anatoka kwa Mungu hivyo tuna wana wawili wa Mungu yaani Yesu na Roho. Aliona kwa hakika Roho Mtakatifu ameumbwa na Mungu ili ahudumu. Amedhibitisha hayo kwa mstari wa Biblia (Yohana 1:3. 4). **Arius** naye

[1] Justo L Gonzalez, *The Story of Christianity: The Early Church to the Dawn of the Reformation,* Vol. 1(San Fransisco: Harper Collins, 1984),76.

[2] Tim Dowley, (ed.), *Introduction to the History of Christianity: First Century to the Present Day.* (Minneapolis: Fortress Press, 2002), 113.

alisema, Yesu Kristo na Roho Mtakatifu ni viumbe tu kama wengine isipokuwa amepewa uwezo wa kipekee na Mungu
Wazee wetu **Athanasio na Tertullian**o walimaliza mjadala wa Yesu Kristo ni Mungu kweli na mwanadamu kweli na kuwa Roho Mtakatifu anafanya kazi na Mungu na ni Mungu (Yohana 4: 24) na aliumba hata malaika hivyo hastahili kulinganishwa na Malaika. Yeye ni nafsi katika Mungu wa Utatu. Kwa kweli ndiye huyu aliyeanzisha fundisho la **Mungu wa Utatu** lililoko katika kiri zetu hadi leo ndani ya Kanisa letu.[3]

Mikutano ya Nices 325 na Nikea Constantinopole ya 381 ndiyo iliyosawazisha maswali yaliyokuwa yameibuka kwa kutokeza imani/kiri na Mitume na ile ya Nikea tulizonazo leo. Hali ya Kupoa kwa Kanisa ikatulizwa kidogo na kanisa likaamshwa. Kukaweko na maelewano na Injili ikaendelea kuhubiriwa.

Kupoa na kuamka kwa kanisa  yaliendelea sana katika historia ya Kanisa, lakini kilikuja kipindi kingine mashuhuri katika historia kile cha matengenezo. Hapa Kanisa lilipoa kwa kukosa dira na muelekeo wake. Utamaduni, Uanadamu kwa watumishi wa Mungu ulifunika utakatifu na utume wa Kanisa. Kanisa likawa kama limemwagiwa maji ya barafu na halikupoa tu bali lilikaribia kuganganda. Watumishi wa Mungu  tunaowaita wana matengenezo waliamshwa kwanza.

Martin Luther kwa kuwezeshwa na Roho Mtakatifu alianza kuona Neno la Mungu kwa utofauti. Luther alikiri kuwa, baada ya kufunuliwa kwa upya maandiko toka Rumi 1:16, ‘nilijisikia kuwa mdhambi mbele za Mungu na hakika nilikuwa sina dhamiri. Sikuwa naona kuwa amenikomboa, sikuwa na Upendo. Nilimchukia huyu Mungu wa haki ambaye aliadhibu wadhambi, na kwa siri nilimchukia Mungu sababu aliifanya dhamiri yangu kila mara isiwe na uhakika wa imani yangu. Baada ya kuona kwa upya mistari hiyo ndipo nikaanza kujihisisha na “Mwenye haki ataishi kwa Imani” na hapo ndipo nikaanza kuelewa.’[4]

Aliona madhara ya kuupokea Ukristo wa kinadharia tu. (Humanism/ scholasticism)[5] aliamka na baadaye akapewa nguvu pamoja na wenzake wakaliamsha Kanisa. Tena niseme ingawa utamaduni wa Kilutheri umetufundisha vyuoni kuwa baada ya mikutano ya akina Martin Luther na Cajetan, basi Luther alitengwa, lakini ndani ya Kitabu cha ‘Concordia’[6] kuna habari za Maandiko ya Kismalaldi. Maandiko ambayo yanaeleza kwamba baada ya Walutheri na wa Rumi Katoliki kutengana, bado Luther na wenziwe waliombwa waseme mambo ambayo wanafikiri yanaweza kuendelezwa kushirikiana katika Kanisa la Kikatholiki na la kimatengenezo.

Na wakati huo huo Kardinali Contarini pamoja na wenziwe walimuandikia Papa waraka uitwao “ *Concilium de emendanda ecclesia*” kusema kuwa hata ndani ya Warumi Katoliki wanahitaji kuliamsha na kulitengeneza Kanisa, walisema, nanukuu: “Wale wanaomdanganya Papa wamemfanya kuamini kuwa mapenzi yao ni kama sheria na wanaweza kushawishi papa kufanya lolote hata kulidhihaki Kanisa. Kwa hiyo hapo baadaye tunaomba papa ubariki wale tu

[3] Dowley, Ibid., 112.
[4] Luther, *LW,* Vol. 34. 337

[5] Stanley J. Grenz, et, ala., *The Pocket Dictionary of Theological Terms.*( Illinois:Intervarsity Press,1999), 106.
[6] Faith K. Lugazia, “The Relevance of Smalcald Articles in Tanzanian Christianity, Andiko lililosomwa katika Mkutano wa Smalkadia, Ujerumani 23, 2012 (Halijachapwa).

walionasifa za kutunza roho za watu na si kushikilia huduma ya kukuongezea papa mapato ya kanisa. Walimalizia maneno yao wakisema kuwa "ni hekima sana kwa kanisa kujishughulisha na matengenezo na kuliamsha kanisa badala ya kukaa wakitetea kila tendo atendalo Papa."[7]

Basi hata ndani ya Kanisa la Kirumi Katoliki uamsho na matengenezo vilitokea. Mengi yalibadilishwa lakini zaidi mwaka 1999, hata fundisho la Kuokolewa kwa neema kwa njia ya Imani - mafundisho ya mtazamo wetu Walutheri, limekubaliwa kuwa ni fundisho sahihi na Warumi Katoliki.[8]

**MADHUMUNI YA ANDIKO**

Andiko hili, si maelezo juu ya historia ya uamsho katika Kanisa bali linalenga sana kuelekeza habari za uamsho ndani ya Kanisa letu la Kiinjili Kilutheri Tanzania. Hivyo litaanza kueleza maana ya Uamsho, Chimbuko la Uamsho ndani ya Kanisa letu. Uzuri wake na Mapungufu yake.

Andiko hili litazama sana katika Uamsho tulio nao leo ndani ya Kanisa letu na Changamoto zake. Andiko pia litaelekeza maeneo ya kushughulikia wakati tunaendeleza Uamsho ndani ya kanisa letu na baada ya hapo tutashirikiana kujadili andiko hili kwa afya na uamsho wa kanisa letu la KKKT.

**UAMSHO NI NINI?**

Katika Dictionary ya *Consice Oxford English Dictionary, Revive - Kuamsha ni "* kurudisha ama kupata tena maisha, kujitambua ama kupata nguvu mpya. Ama kujirekebisha kutoka katika hali mbaya kuelekea katika hali nzuri.[9]

Kikristo, I. Packer: "Amesema kuwa Umasho ni kuja haraka kwa Mungu, kuwatembelea watu wake, kugusa mioyo yao na kuongeza utendaji wa neema yake kwa watu wake".[10]

Robert Baird, yeye anasema Uamsho "ni muda/ kipindi maalum unaopenda kushughulika na mambo ya dini/ Imani."[11]

Na J. Edwin, yeye anaona kuwa "Uamsho ni muda wa wauminin kujiangalia kwa upya juu ya uwepo wa Mungu kwa kanisa lake (Matendo 3: 19)."[12]

Ninapenda kwenda na ufafanuzi wa Edwin kwa sababu anazungumzia uamsho kuwa unafanyika ndani ya waumini tayari lakini zaidi ni Mkristo anayechukua hatua baada ya kujitathmini ahadi yake kwa Mungu na utekelezaji wa ahadi hiyo. Na hivyo tunapozungumzia Kanisa letu la KKKT na uamsho tunataka kusema kuwa Tumejitathmini na kuona tunahitaji kwa upya kuona uhusiano wetu na Mungu unathaminika kwa kukiri uwepo wa Mungu katikati yetu.

**HISTORIA YA UAMSHO NDANI YA KANISA LETU**

---

[7] William Placher, *A History of Christian theology: An Introduction. (*Pennsylvania: Westminster press, 1983), 201

*8 "Joint Declaration on the Doctrine of Justification". Pontifical Council for Promoting Christian Unity. 31 October 1999.* ( Retrieved 2014-01-17.*)*

[9] *The Concise Oxford English Dictionary, 11th Ed. 2004.* 1232.

[10] J. I. Packer, *Revival: Rediscovering the Holiness: Knowing the Fullness of Life with God, 2009*

[11] Robert Baird

[12] J. Edwin Orr, *Evangelical awakening in Africa,* (Minneapolis: Bethany Fellowship, 1975)

Uamsho basi unatokea pale ambapo Kanisa linakiri kuwa kuna hali ya kulala ama kulegea kwake kwa mambo kadhaa ya kiimani na kimatendo kwa ujumla, nikitumia lugha ya kimatengenezo ni kuona kuwa kuna hali ya kutoweka katika mizania ya usawa "**INJILI na SHERIA**."[13]

Pamoja na mabadiliko tunayoyaona leo ndani ya Kanisa letu la KKKT, chimbuko la uamsho hapa kwetu ni pale Gahini nchini Rwanda ndani ya shule ya Kianglikana. Shule hii ilikuwa chini ya wamisionari kutoka CMS. Wamisionari hawa walikuwa na makao makuu pale Uganda ila walianzisha shule hii kwani walikuwa wamepata hamasa ya kufanya kazi ya umisioni pia Rwanda. Kilichotokea ni kuwa mabinti kadhaa wa shule ya kati walipokuwa katika sala ya jioni mara ghafla wakashukiwa na nguvu ya Roho Mtakatifu. Badala ya kunena kwa lugha kama tunavyosikia kwa makundi mengine, mabinti hawa walifunuliwa dhambi zao, wakaonyeshwa kuwa walikuwa wanamkiri Yesu katika midomo yao lakini ndani mwao walikuwa wachafu.

Walikuwa waongo, walikuwa wakisengenyana, walikuwa wazinzi na hata walikuwa wakiibiana. Waliishi maisha ya unafiki kwa kutopendana ama kutokushirikiana mara baada ya matendo ya ibada kama sala na mengine. Ndipo walipoamua kuchukua hatua ya **kutubu**. Walitubiana kati yao. Walirudishiana yale waliyodhulumiana[14], waliombana misamaha na **kutengeneza** mahusiano yaliyokuwa yameharibika. Na baada ya hapo wakaamua kuchukua hatua za **kutembea nuruni:** yaani kuelezana yale wanayopanga kufanya iwe ndani ya familia, shule na hata ndani ya jamii[15]. Matendo ambayo baba askofu E. Sendoro Senior, anayaita tabia za uamsho wa Afrika Mashariki.[16]

Habari hizi zilienda moja kwa moja hadi kituo cha Umisioni cha kanisa la Kianglikana na kutoka Uganda zilienea Kenya na Tanzania. Na Tanzania zilianzia Bukoba na Dodoma ambapo mmoja wa wana umasho huo Askofu Festo Kivengere alifundisha katika shule ya Kianglikana ya Alliance, Dodoma na baadaye kuhudumu baada ya kuwa mchungaji na kuhubiri sana nchini Tanzania kupitia AEE.

Uamsho huu ulipoingia ndani ya Kanisa letu ulipokelewa na wengi na hakika wengi ndani ya Kanisa letu, waliendea maisha ya "Uamsho wa Afrika Mashariki." Makundi ambayo tumeyaita ya wana 'fellowship' ndani ya Kanisa letu ndiyo makundi yaliyozaliwa na uamsho wa Afrika Mashariki.

**Uzuri wa Makundi haya:**
Yalikubali kubaki ndani ya Kanisa. Mch. Dkt. W. Niwagila akitumia lugha ya Kilatini, aliyaita makundi haya "Ecclesiola in Ecclesia"[17] akimaanisha kuwa ni makundi ambayo yamekuwa

[13] D. Bernhard Lohse, *Martin Luther's theology: Its Historical and Systematic Development, (*Minneapolis: Fortress Press, 1999) , 269 cf. *WA, 391, 416, 8-14*

[14] katika mahojiano yake na Mch.Sylvester Machumu anaripori kuwa: katika Mkutano wa Dayosisi wa mwaka 1938 pale Butainamwa, kundi la Wanyarwanda walifika pale kutoka Rwanda kuja kurudisha vitu walivyokuwa wameiba na hata kutubu kutokuwa waaminifu ndani ya huduma yao. Toba yao iliambatana na machozi na kupondeka na kujutia dhambi yao. Katika Samson B, Mushemba, "The History of the Revival Movement in the ELCT-NWD, St. Paul, Minnesota, 1982" 56.

[15] Mahojiano na Can. Patrick Butera na Canon Joseph Kayumbu, Gahini Parish, Aprili 26th, 2016

[16] Elinaza Sendoro, *Uamsho na Karama: Roho Mtakatifu katika Makanisa ya Kihistoria.* ( Moshi: Millenium Books, 2000)

[17] Wilson Niwagila, From the Catacomb to the Self Governing Church

kama makanisa madogo ndani ya Kanisa. Makanisa haya madogo yameendelea kuamsha kanisa kwa kulikumbusha wito wake hasa kwa habari ya kulifanya Neno la Mungu kuwa chimbuko la huduma yake yote ya kimisioni na zaidi sana kuliombea Kanisa na watumishi wake.

Mch. Dkt. Annete Munga ameendelea kuyashukuru makundi haya kwa kusema kuwa 'ingawa hayakuingia darasa la theologia, lakini yanafundisha kuwa kuokoka ni mchakato ambapo katika mchakato huo, mwanadamu anachukua hatua madhubuti chini ya ulinzi na uongozi wa Kristo[18] unaomtaka mtu kukiri kwa kinywa chake kuwa ameokolewa na Kristo na mara zote kutembea na kuishi katika ukiri wake.'

Mch. Dkt. Josephat Rweyemamu anasema, uamsho wa Afrika Mashariki, umefanya wakristo kuweka wokovu wao katika matendo na kuwa Biblia ilifafanuliwa kutoka ufahamu wao na hivyo wakaona umaana wa Ukristo.[19]

Bwana Johanssen Lutabingwa akifafanua zaidi alisema kuwa Ukristo wa mwanzo ulisaidia waumini kujifunza katekismo, kusoma na kuandika. Lakini Ulokole (Afrika Mashariki) ulisaidia waumini kujitambua kiimani kwa Kristo waliyemuamini na hata kufanya Ukristo kuwa na maana katika maisha.[20]

Kupitia uamsho huu, waumini walitumia lugha ya imani ambayo ilikuwa ndani ya uzoefu wa maisha yao ya kila siku.[21] Nikitumia maneno ya Harvey Cox, alisema, "waliimba theologia badala ya kulumbana nayo."[22] Na Welbourn akamalizia kwa kusema kuwa,Wakristo walipata uhuru wa kushuhudia Yesu ndani ya makanisa yao na hivyo wakaona kanisa ni mahali poa na wakajisikia nyumbani."[23]

Askofu Dkt. Josiah Kibira, kama mmoja wa mwanachama wa mwanzo katika uamsho huu ulipoingia Bukoba anasema" Uamsho huu umesaidia makanisa ya Afrika kujenga Imani yao katika Mungu, na kuwa Kanisa limejisikia kuitwa kuwa la Kimisionari kwa ajili ya Kristo."[24] Na uamsho umejenga Umoja ambao umeenezwa sehemu kubwa ya dunia na wana uamsho hawa."[25]

Uamsho huu, ulishirikisha wanaume, wanawake na vijana katika kumshuhudia Kristo na kazi yake ya kutukomboa kwani makundi haya hayakuhitaji vigezo vingine kama elimu ama miongozo mingine ya kuwafanya wao kushiriki misioni ya Kristo. Walishiriki kikamilifu na kupitia wao, Kristo alihubiriwa na watu walikuja kwa Yesu kwa kuponywa roho zao na miili

[18]Anneth, Munga, A *Theological Study of the Proclamation of the Revival Movement within the Evangelical Lutheran Church in Tanzania,* (Lund: Lund University Press, 1998), 89.

[19] Josephat Rweyemamu, *Convention Discourse in African Perspective.*(Kamen: Hartmut Spenner, 2014) 235

[20]Bengt, Sundkler, *Bara Bukoba: Church and Community in Tanzania.(*London: C. Hutst, 1980), 128

[22] Harvey, Cox: *Fire from Heaven: The Rise of Pentecostal Spirituality and the Reshaping of Religion in the 21st Century.*(Reading, Maddison-Wesley, 1996), 18

[23] F. Welbourn, *East Africa Rebels.*(London: Oxford University Press,1962), 205

[24] Josiah M. Kibira, *Church, Clan and the World.*( Uppsala: Almquist and Wiksell,1974), 56.

[25] Russel Chandram, "Report on the Faith and Order Working Committee on the *Church Union Conversation, Limuru Kenya"* Minutes of the Faith and Order Commission, Geneva, 1962, 45-46.

yao. Aidha ushiriki wao wa uaminifu katika Kanisa ninadiriki kusema ndio kumetoa ushuhuda wa Kanisa la Kilutheri hapa Tanzania. Wachungaji na watumishi wengi ni watoto/ wajukuu wa wana uamsho wa Afrika Mashariki.

Niongeze kwa kusema kuwa Dkt. S. Mushemba amesema: "Uamsho wa Afrika Mashariki uliweka moja ya utambulisho wetu; Ukuhani kwa wote waaminio katika matendo." Kanisa liliwashirikisha waumini wake pasipo kujali jinsi, cheo wala rangi. Wote walikuwa wamoja. Wimbo wao ulikuwa: **TUKUTENDEREZA YESU.**

**Mapungufu ya Uamsho wa Afrika Mashariki.**
Wana uchumi husema kuwa kila kitu chenye faida kina hasara pia. Ingawa uamsho huu uliwavuta wengi kwa Yesu na kulifanya Kanisa kuwa la wenyeji, wapo wengine waliona uamsho huu kuwa ulikazia sana matendo na si Imani.[26]

Wanaumasho walitakiwa kujitahidi kukumbatia amri za "usi, usi, uki uta.." na hata Mchg. Simeon Kabugumila anasema kuwa kwa kweli pamoja na uzuri wa uamsho huu lakini walikuwa na hukumu sana juu ya matendo ya wengine na hata kupenda kuona wokovu kama ni jambo la ubinafsi na hivyo kuleta mgawanyiko ndani ya kanisa moja.[27]

Wana 'fellowship' walijitenga kiasi cha kuona waumini wengine ndani ya Kanisa moja kama si wakristo. Bwana Josiah R. Mlahagwa, anahakikisha ukweli huu kwa kusema kuwa, mgawanyiko huo ulitokea kwa aina mbili. Kuna wakati ambapo wana uamsho waliona kuwa mchungaji hana maana sana kwao bali kiongozi wa "fellowship" na wakati mwingine "fellowship" ilipoacha kutegemea chochote kama msaada toka usharika, viongozi wa "fellowship" walimuona Mchungaji kama hana maana kwao. Akaongeza kuwa mnakumbuka vurugu za Magomeni mwaka 1996.[28]

Mfano mwingine unatolewa kwa mambo ya maadili yaliyolenga kuwanyima haki wanawake kuwa,Wanawake walilazimika kutojipamba na hata kutoruhusiwa kupaka mafuta ili wasitamanishe wanaume.[29] Hata mavazi yao yaliratibiwa. Suala la mavazi ambalo hadi leo limeendelea kuwa swali kwa Kanisa letu. Na wanawake wanahukumiwa zaidi kwa mavazi yao kuwadhuru wanaume kana kwamba wanawake hawakuumbwa na tamaa ya mwili na hivyo hawadhuriki inapokuja kwa mavazi ya upande wa wenzao wanaume. Ushuhuda wa wazi hasa ulioelekeza makosa ya uzinzi kwa wake ama waume walio katika ndoa ulileta uhasama zaidi ya upatanisho.[30] Niendelee kusema pia Uamsho huu unapoangaliwa kitheolojia ulionekana kuwa na mapungufu yake.

[26] Niwagila,*From Cata-Comb…* 248.
[27] Simeon Kabugumila,"Conversion and Revival:A Critical Analysis of the Revival Movement among Lutheran Christians in North Western Diocese of the Evangelical Lutheran Church in Tanzania." (Unpublished:PhD Dissertation. University of Kwazulu Natal, Pietrmaritzburg, 2005),132-141.
[28] Josiah R. Mlahagwa, "Contending for the Faith: Spiritual Revival and the Fellowship Church in Tanzania" in *East African Expression of Christianity. Thomas Spear and Isaria Kimambo (eds.,)* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota,1999.
[29] Niwagila, *from the Cata-Comb.*
[30] Niwagila, Ibid., 250

Mafundisho yake yalitenga Utendaji wa Utatu Mtakatifu: Yalidhani kukaza utendaji wa Roho Mtakatifu,[31] kisha Yesu, na kushindwa kuingia katika nafasi na kazi ya Mungu Baba; kwamba wao wameumbwa tena kwa mfano wa Mungu ili wapende wenzao na kumhudumia, haikuwa ajenda kwao. Ajenda kubwa ilikuwa **uokoke ndani ya damu ya Yesu** na ukishaokoka basi mlokole mwenzio atakupenda na kukuhudumia lakini si nje ya "inner circle" ya walokole.

Mume wangu ambaye baba yake na baba yake mkubwa walikuwa wana uamsho wa Afrika Mashariki katika hili anasema: "ubaya wa ulokole huu ndani ya ukoo wetu ni kuwa undugu wa kibaiolojia haukuwa na nafasi kwa undugu wa kikristo. Kuwa wazazi wetu walitutambulisha na kutuungamanisha na walokole wenzao zaidi ya ndugu zao wa damu." Hali hii imeathiri sana sisi watoto kwani ni watoto wa baba mkubwa mmoja tu ambao tunawasiliana hadi leo vema na si watoto wa baba wakubwa wengine."[32]

Ulileta swali kubwa kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu kwa waumini na Kanisa.[33] Hawakufundisha sana kazi ya Roho Mtakatifu kuhusu kutoa karama za kulijenga kanisa. Bali hawa walijua kuwa kazi ya Roho Mtakatifu ni kukushuhudia ukweli wa maisha yako na uhusiano wako na Yesu ili utubu pale ulipokosa na utangeneze. Yaani Roho Mt. alidhaniwa kufanya kazi na mtu mmoja mmoja. Kwani Roho Mtakatifu alionekana kuwa ni nafsi ya Mungu ambayo yaweza kutawaliwa na utashi wa mwanadamu na kwamba Neno linapohubiriwa ni lazima mtu atubu dhambi na kuokoka.

**Sakramenti za Kanisa zilipuuzwa** na **kukiri hadharani** kukapata nafasi kubwa zaidi ya ubatizo. Baadhi walisikiwa wakishuhudia kuwa walibatizwa na kukaa kanisani kwa muda mrefu bila ya kukutana na Bwana Yesu - mafundisho ambayo hadi leo yanaleta mkanganyiko mkubwa kwa waumini wetu.[34] Swali kubwa limeendelea kuwa je kuokoka na kusimama mbele za watu na kutubu dhambi zako hadharani ama ni kubatizwa katika Utatu Mtakatifu? (Marko 16: 16 - 19); ama ni habari ya kumkubali, kumtengemea na kumwamini Kristo aliyekufa na kufufuka kwa ajili ya dhambi zetu?[35]

**Njia za kutafsiri/ kuwa na matafakuri** ya Biblia **(Biblical Exegesis and hermeneutics)** kwao hazikupata nafasi kubwa bali walitumia sana njia ya kulinganisha mifano (allegory) ili kufikisha ujumbe [36] Hivyo mara nyingi walijikuta wakitumia sehemu ya Biblia kujihesabia wokovu kwa kuwa wameacha kutenda matendo fulani fulani yaliyohesabika mabaya kimaadili.

Nifunge sehemu hii kwa kusema kuwa uanadamu na ubinafsi uliingia ndani ya makundi hayo na wakawa na tamaa za mambo mengine /dunia kama kutaka vyeo na madaraka. Ama kutokubali kunyenyekea katika kuongozwa na hata wengine walio na uongozi wa Kanisa, unayatawala makundi hayo sana. Hivyo msukosuko huu ukaleta kupoa kwa kanisa letu kwa sehemu.

---

[31] Fidon Mwombeki, "Roho Mtakatifu" katika *Wakristo Tusemezane* (Morogoro: CCT Literature Department, 1988), 6.

[32] Maongezi na Bw. Joeivan Kataraia, (June,2015)

[33] Bengt Sunkler, *Bara Bukoba*, 47

[34] Mushemba, "The History…" ,62, Kibira, *"Church Clan…"* 40-41

[35] Niwagila, *Catacomb - 254.*

[36] George K. Mambo, *The Revival fellowship (Brethren) in Kenya.* (Kenyan Churches Handbook, Kisumu, 1973) 10 - 24.

**Mchango Wetu katika Kupoa kwa Uamsho wa Afrika Mashariki**

Kwa upande wa Kanisa la Kilutheri tulipata changamoto kutoka kikundi hiki kwani Wachungaji waliokuwa bado kukiri wazi kuwa wameokolewa, kwa mtindo wa uamsho huu, walipenda sana kuangalia madhaifu ya vikundi hivi zaidi ya uzuri wa vikundi. Pili, kwa vile Wachungaji walijiona kuwa na madaraka kama viongozi, basi waliingia katika mvutano, magomvi na vurugu. Baadhi ya Wachungaji walifukuza kabisa vikundi hivyo ndani ya sharika zao.[37] Kwa hali hiyo niseme Kanisa letu likapoa kwani habari ya utume wake wa kufundisha na kuhubiri vikakosa ushuhuda.

Niongeze kusema kuwa wakati hayo yakitokea, Kanisa letu kwa ujumla wake lilikosa kutoa mafundisho yake ya msingi na badala yake likaingia katika malumbano. Mijadala mingi kuhusu makundi haya na mafundisho yake ilikuwa ikitetea uongozi wa kanisa na kuwa wale waumini wanakosea badala ya kujiuliza kuwa ni wapi tumekosea hadi waumini wetu wanatokeza mambo haya tuyaonayo? Kukosa mafundisho niseme nako kumechangia sana hali halisi ya Ukristo tulionao leo ndani ya Kanisa la Kilutheri.[38] Badala ya kukazia mafundisho kwa waumini, sisi watheolojia tukakaza kujihesabia haki na kuwaona wale hawajui mafundisho ya Kuokolewa kwa Neema. **Ambapo binafsi najiuliza swali kuwa hivi kweli wengi wetu tunafahamu fundisho hili kwa maana ya Martin Luther?**

Mfano Mchg. Naaman Laizer anasema katika Wokovu wa mwanadamu kwamba mwanadamu si mtendewa tu, bali kuna jinsi anavyoshiriki ndani ya uwezo na mpango wa Mungu.[39] Ushiriki wa muumini ni nini hapa? Askofu Josiah Kibirah anasema kuwa Wachungaji wetu na hata Wainjilisti hawawezi kuelezea kwa kina fundisho hili la kuokolewa kwa Neema kwa njia ya Imani.[40]

Mtumishi Prof. Mika Vahakanga's anakubali hoja ya Kibira kutoka utafiti wake. Kwa maelezo yake anasema, "Utamaduni wa Mtanzania kufuatana na maelezo ya wanafunzi kutokana na utafiti aliofanya pale Makumira unaonyesha kuwa matendo ya neema hayafahamiki kwao. Wao wanamjua Mungu anayemtaka mwanadamu kufuata masharti yake na kinyume chake ama badala yake ni kuadhibiwa." Hivyo katika maisha ya kawaida ya kanisa, tunakaza sana sheria."[41] Na akashauri ilivyo katika utamaduni wa magharibi ni muhimu kutambua kuwa "Soksi ya saizi moja haiwezi ikawatosha watu wote"[42] Wasomi hawa wote wanaonyesha ni kwa jinsi gani urithi wetu haujapakuliwa vya kutosha ama haujaingia katika mazingira na ufahamu wetu kama Waafrika na ndiyo sababu Kanisa limekuwa moja ya sababu ya kuleta mkanganyiko na maswali yaliyoko Kanisani kwetu leo.

[37] Mlahagwa, Ibid. 300

[38] Wachungaji tumelaumu wakristo wetu kwa kujiunga na makundi mapya ya uamsho lakini tunasahau kuwa wengi wa watu wetu hawana uhakika na mafundisho yetu. Kwa mfano juu ya Roho Mtakatifu.

[39] Naaman Laiser, "The Communion of God and Man in the Holy Spirit: A Study of the Concept of the Holy Spirit in Contemporary Lutheran Thinking" (Th. D. Diss., Hamburg, 1981), 29, 31.

[40] Josia M. Kibirah, "Has Luther Reached Africa: The Testimony of a Confused Lutheran" in ATJ, 12: 1 (1983) 6-15

[41] Mika Vahakangas, "Teaching Lutheran Theology in Tanzania - On the (Ir) Relevance of Lutheran Theology, in *Dialog: A Journal of Theology.* Vol.42. (2), 2008, 171 - 174

[42] Vahakanga's Ibid.

Niseme pia kwa mafundisho haya yetu bado tamaduni mbili, ile ya kimagharibi ambayo ina uhuru wa kupitiliza na hayo ya kwetu ambayo mipaka yake ya uhuru bado imo ndani ya sheria za kiutamaduni "USI", "uki .... uta" (apodictic laws).

Matengenezo ya Kanisa hapa kwetu hayana budi kuingilia kwa juhudi zote jinsi ya kumkomboa Mtanzania kutoka katika mvutano alionao wa 'nitii mila na maswali yaliyoko ndani ya jamii yangu leo ama mila za utamaduni na malumbano ya Karne ya 16 ndani ya jamii ya Kimagharibi'.[43]

Pamoja na sababu hii ya kupoa, Tanzania pia tukaingia katika kipindi kigumu, miaka ya 1970 - 1980

**KILICHO SABABISHA WAUMINI/ KANISA KUPOA NA KUANZA KWA UMASHO MPYA NDANI YA KANISA LETU**

Katikati ya kupoa kwa kanisa hapa kwetu Tanzania, kwa sababu ya kukosa mafundisho ya msingi ya urithi wetu na "siasa za Kanisa", ambazo nimezitaja hapo juu, tukapata matatizo mengine ya kijamii na kiuchumi ambayo nimeyaorodhesha hapa chini:

- Tanzania tuliingia katika vita na Uganda 1972 na 1978 kuhusu sehemu ya Kagera, ambapo Rais wa wakati ule wa Uganda Idd Amin alipenda sehemu ya Kagera iwe yake. Watanzania tulikataa na kufuata kauli mbiu ya Mwl. Julius Kambarage Nyerere kwamba "tumtokomeze huyu Amin kwa sababu: Uwezo tunao; Nia tunayo na Sababu tunayo."[44] Nguvu zote za uchumi zikaelekezwa vitani. Askofu Bengt Sundkler anaripoti kuwa: "Vita vya Tanzania na Amin viligharimu Tanzania Dola za Kimarekani milioni 500 ambazo kwa wakati huo ilikuwa zaidi ya mapato ya mwaka kwa Serikali yetu."[45] Fedha ikawa adimu nchini na umaskini ukaongezeka.
- Nchi za ghuba zilisitisha biashara yake ya mafuta, na hivyo viwanda vingi hapa kwetu vikafungwa.

Matatizo hayo mawili niliyotaja yalisababisha si tu mazao kuharibika lakini pia yalisababisha na thamani ya shilingi kushuka kwa kiasi kikubwa. Wakulima na wafanyakazi walijiona kuwa kama wametelekezwa na hivyo ikawabidi watafute njia zao za kujipatia riziki ili waweze kuishi."[46]

- Kana kwamba changamoto hizo hazitoshi ukaingia ugonjwa wa Ukimwi. Kwa vile ilikuwa ikisadikiwa kuwa ni ugonjwa wa uzinzi na laana kutoka kwa Mungu, Kanisa halikujihusisha nao. Mwaka 1983, utafiti ulipoanza kufanywa na Serikali na mwaka 1996, Program ya kuthibiti Ukimwi ya taifa iligundua kuwa tayari Watanzani 88,667 wana virus vya UKIMWI, kufikia miaka ya 1990, idadi ilipanda hadi 600,000 na kufanya idadi hii kuwa kubwa kuliko

[43] Ninasema maneno haya kutokana na ukweli kuwa urithi wetu kwa kiasi kikubwa umetawaliwa na matokeo ya malumbano yaliyokuweko katika jamii ya Martin Luther. Mfano fundisho la "Injili na sheria", *WA 391, 361, 1-6.*

[44] Hotuba ya Mwl. Julius Kambarage Nyerere ya 2November, 1978 pale Diamond Jubilee. http://www.jamhurimedia.co.tz/uwezo-wa-kumpiga-tunao-sababu-ya-kumpiga-tunayo/ (accessed 15,May,2016)

[45] Bengt Sundkler and Christopher Steed, *A History of the Church in Africa* (Cambridge: Cambridge University Press, 2000), 1012

[46] Sundkler, *A History,* 1012

> nchi zote za Afrika mashariki na kati."[47] Pia utafiti ulionyesha kuwa hadi mwaka 2001, Tanzania tulikuwa na watu 2,220,000 walioishi na virusi vya UKIMWI. Watu 140,000 walikufa kwa UKIMWI na kuacha watoto yatima wapatao 810,000".[48]

Changamoto hizi zoote, zilimfanya Mtanzania kukanganyikiwa.[49]

Makanisa yalionekana kama yamepoa kwani Injili iliyokuwa ikihubiriwa, haikujibu kwa haraka maswali na mahitaji ya watu kwa wakati huo. Ni wakati huo pia, yaliingia makundi ya wahubiri (Injili) yaliyodai kutoa majibu ya maswali ya Watanzania. Yalikaza kuhusu hukumu na hatari ya kuchomwa vibaya kwenye moto wa milele kwa yule akataaye kutubu. Mfano yalijiita makundi yanayotoa Injili Kamili; ama makanisa au vikundi ya uamsho vinavyofundisha na kutoa wokovu wa kweli; Makundi ya maisha mapya, nk.

**UAMSHO TULIONAO NDANI YA KANISA LETU LEO**

Nianze sehemu hii nikiendeleza sehemu niliyomaliza nayo kuhusu makundi ya uamsho wa Afrika Mashariki. Baada ya yale yaliyotokea kanisani na ndani ya taifa letu. Maamuzi ya vikundi vya uamsho wa Afrika Mashariki ndani ya Kanisa letu **yalikuwa mawili**:

**Uamuzi wa kwanza** ulikuwa ni kuongeza huduma zilizokuwa zikitolewa na makundi ama makanisa mapya ndani ya makundi yaliyokuwa ndani ya Kanisa letu ili waumini wetu wasiondoke na kujiunga na makundi yale[50]. Huduma zilizokuwa zikitolewa na makundi mapya/ ama makanisa mapya ni kama maombi na maombezi kwa wagonjwa, kunena kwa lugha kwa walio na karama hiyo na kutoa unabii. Baadaye yakaongezwa, Mafundisho kuhusu mapepo, mashetani, vinyamkera, nk. Mafundisho pia yaliendelea kuongezwa kadiri vikundi hivyo vilivyoona hitaji. Mfano leo tuna mafundisho ya utajiri wa afya na mali (prosperity gospel), mizimu ya mababu na jinsi vinavyotesa watu na jinsi ya kushughulika navyo. Makundi haya ndiyo yanaitwa ya **kikarismatiki**[51] ndani ya Kanisa letu.

J. R. Mlahagwa anasema, Uongozi wa wakati huo wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani akina Baba Askofu Sendoro Senior, na Mch. Yohana Marko waliuga mkono huduma hizi kutendeka ndani ya Kanisa letu.[52] Wasomi kadhaa wameona kuwa kwa kukubali kuongeza haduma hizi kwa makundi haya ndipo urithi wetu wa Kilutheri ulipotelekezwa[53]. Hata wengine wanashangaa

---

[47] "Strategic Framework for the Third Medium Term Plan (MTP-111) for the Prevention and Control of HIV/AIDS/STDs 1998-2002" (Ministry of Health: Tanzania Mainland, 1998), 2.

[48] UNAIDS/WHO, "Epidemiological Fact Sheets on HIV/AIDS and STD Infections," Tanzania 2002 Update.

[49] Faith K. Lugazia, "Charismatic Movement and the Evangelical Lutheran Church in Tanzania" in .*Charismatic Renewal in Africa: A Challenge for African Christianity.* Mika Vahakangas and Andrew, Kyomo. (eds.,) Nairobi: Acton Publishers, 2003, 45-65.

[50] Faith K. Lugazia," The Challenges of Charismatic Movement in the ELCT and the Need for Cooperation: A Case of the ELCT/ Eastern and Coastal Diocese" Master's Thesis. St. Paul Minnesota, 2001.

[51] Faith K. Lugazia, "Charismatic Movement…ibid.,

[52] Mlahagwa, "Contending for the Faith…," 302.

[53] Mlahagwa,299-230 anaeleza jinsi makanisa ya Kiprotestant yalivyoungana na kuweka azimio kukataza watu kuja hubiri kanisani, ama wa kwetu kwenda kwao kuhubiri, na kuwa ikifanyika moja kati ya hilo mkristo wetu atakuwa amejinyima haki ya Ulutheri

kuwa "mbona huduma hizi zilipotolewa ndipo dhana ya nguvu za giza na nguvu zake kama mapepo, mashetani, mizimu, vinyamkera, nk., ndani ya Kanisa letu ndipo viliongezeka?"[54]

Lakini mimi, Prof. Peter Kijanga, Dkt. Josephat Rweyemamu[55] na wengine ambao maandiko yao hayajawekwa katika maktaba ama maduka ya vitabu, tunakubali kuwa kwa kuunga mkono huduma hizo Kanisa letu halijatelekeza urithi wetu bali tunakabili changamoto hii ili tuweze kutokeza mafundisho/ huduma nzuri kwa Ulutheri wetu.

Katika jopo la watheologia lililokutana kule Lyamungo,(2003) nilisema: "Makundi haya ni changamoto kwa Kanisa letu na tunahitaji kukaa pamoja kujadili (dialogue) badala ya kubezana na kulaumiana kwani katika habari za Imani na kumfahamu Kristo wote tunahitaji kufundishana maana hakuna aliye na ukweli wote.[56] Ni Yesu pekee aliyenao (Yohana 18:37). Wote kama Pilato tunamuuliza Yesu: "Ukweli ni nini?"

Prof. Kijanga, alishauri kuwa jambo la uamsho (huu wa kileo) lisipokelewe kwa unafiki au kwa woga ili tu kuwapendeza watu fulani au hali fulani na wala hatuwezi kukanusha suala hili zima la uamsho kwa kusema jambo hili halipo wala haliwezekani. Bali tuwasaidie watu wetu kwa kukazia mafundisho.[57]

Hivyo katika hili pia niseme tunaugana na viongozi hawa wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani kukubali kuwa Kanisa limeitwa kuwahudumia wote katika hali zao. Kama watu waliathiriwa na matatizo niliyotaja ama walikuwa na matatizo mengine, ninaona kwa kukaribisha huduma hizo ndani ya Kanisa letu watu wameponywa miili, roho na nafsi zao.[58] Wameweza kusimama wenyewe kama waumini na kuwa na roho ya kulitumikia Kanisa. Pia ndani ya kanisa tumepata watu ambao bado ni wanachama wa kanisa letu lakini wana huduma nje ya kanisa (ministries). Manna ministry[59] ni moja ya hizo.

Lakini maamuzi ya pili yakawa ni kuanzisha madhehebu/ makanisa yao. Wahubiri mashuhuri tunaowaona leo ama katika runinga ama pengine, yametokana ama yanaongozwa na wakristo wetu. Kule Kilimanjaro, tunamkumbuka sana Mwj. Emanuel Lazaro aliyekuja kufanya kazi na Mwjl. Mosses Kulola. Kule Bukoba kanisa kubwa la wale waliochukua hatua ya kutoka kwetu na kuanzisha kanisa (Rhema Church) ni mtoto wa Mchungaji wetu (Lutheran), mume, na mke ni

[54] Wilson K. Lugakingira, "Kanisa na Umasho"- Andiko kwa Mkutano wa Wachungaji Morogoro, 1997" Halijachapishwa.

[55] Yeye anasema kuwa makundi haya yamejitahidi sana kujibu maswali magumu yaliyoishi ndani ya waumini kwa muda mrefu wakiogopa kuuliza ama kutaja kwa kile walichofikiri kuwa watakuwa wamevuka mipaka ya mafundisho ya wamisionari. Cf. Josephat Rweyemamu, 252.

[56] Lugazia," Charismatic Movement

[57] Peter Kijanga, "Ubatizo na Roho Mtakatifu" in Essential Essays on Theology in Africa, Arusha: Makumira Publications (5),Ed. Leonidas Kalugila and Nancy Stephenson, 1987), 69.

[58] Lugazia, "Itikio la Changamoto za Vikundi vya Kikarismatiki na Upentekoste kuhusu (Uponyaji na Matendo ya Miujiza) katika Kanisa letu". Andiko nililotoa Makumira, Kama itikio kwa mtoa Mada hii. Mch. Dkt. Msafiri Mbilu, Juni, 2013.

[59] Kikundi cha huduma cha Mwl. Christopher Mwakasege. Msharika wetu pale Kijenge, Dayosisi ya Kaskazini Kati. Pamoja na malalamiko dhidi yake kuwa hajasoma theolojia, Mch. Dkt. Fidon Mwombeki anakiri kuwa, hakuna mtumishi wa Mungu ndani ya KKKT anayefundisha Biblia kuzidi yeye.

mtoto wa Askofu, (Lutheran). Familia hii wanaendelea na huduma yao na namba kubwa ya waumini wao ni wale waliokuwa walutheri. Kwa mfano 'Big November Crusade.'[60]

Katikati ya hayo yote, vikatokea vikundi toka nje, vilivyohubiri na kufundisha uamsho ulio zaidi ya ule wa Afrika Mashariki vilivyofundisha hata nje ya huduma zile nilizotaja awali. Hawa walikuja na huduma ya Injili ya Utajiri wa kimwili na Kiroho (Prosperity Gospel).Wahubiri na walimu wa vikundi hivi wakadai kuwa makanisa mengine ya kihistoria hawana Roho Mtakatifu na ndiyo maana ndani ya makanisa yao hakuna maombi ya uponyaji, matendo ya miujiza, maono ya kinabii na hata kunena kwa lugha ambayo ni alama ya kuupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu na moto. Baadhi wanadiriki kutoa Roho Mtakatifu ndani ya mikoba yao na kuwamwagia watu.[61]

**UAMSHO WETU PIA NI WA KIKARISMATIKI**

**Uamsho wa 'Charismatic' ni nini?** Ni uamsho ndani ya makanisa ya kimisionari wenye tabia kama za Upentekoste[62] wa kileo ambapo viongozi wake wanapewa karama za kufanya matendo ya miujiza.

**TABIA YA WANA UAMSHO HAWA**

Makundi haya yapo ndani ya Kanisa letu. Yanakaza kuwa ni Roho Mtakatifu awawezeshaye kuamini na ni huyo Roho Mtakatifu anayekupa karama kama ukimwomba kwa bidii. Viongozi wake ni Wachungaji wetu. Lakini pia yako makundi ambayo yanaongozwa na raia waumini ndani ya kanisa. Dodoma sina uzoefu nako sana ila Dar es salaam tunaye Mchungaji Wilbroad Mastai, kuna Mwinjilisti pale Kariakoo, Bukoba Mch. Tito Mbekenga, Arusha Mch. Babu wa Loliondo, najua hata sehemu nyingine nyingi tu za KKKT. Niseme pia kule kwetu ambapo ule uamsho wa Afrika Mashariki ulianzia, makundi ya kileo yanaongozwa hasa na vijana wanaodai kuwa wao ni sauti ya mabadiliko. Wana uamsho hawa pia wako kwa wingi ndani ya vyuo vingi ndani ya nchi yetu.

**Mafundisho ya Makundi haya**

Kwa sababu ninasema yako ndani ya kanisa letu hivyo mafundisho yao mengi ni kama yale tuliyozoea kwenye makanisa yetu ila yana tofauti nasi kwa mafafanuzi yao. Na hapa ndipo ninadhani Kanisa letu linapaswa kuwa makini kwa kufundisha yaliyomo ya urithi wetu ili watu wetu wasivutwe na ule mfanano.

**Sakramenti:** Zetu za Ubatizo na Chakula cha Bwana hazina maana sana kwao. Wanadai kwamba hizo ni utaratibu tu wa Kanisa. Kwao wanathamini Toba ya hadharani na baada ya hapo kuishi maisha ya utakaso. Maisha ya matendo yanayoshuhudia ukiri wako.

**Injili ya Utajirisho ( Prosperity/ Gospel/ Theology)**

Asamoah-Gyadu, D. Maxwell, F. Lugazia, P. Gifford na O. Kalu tunakubali kuwa kuna uhusiano kati ya mafundisho ya Kimarekani kuhusu Injili ya utajiri na yale yanayofundishwa na wahubiri

[60] Ibid

[61] Niliona katika runinga, kiongozi wa Kanisa la Mlima wa Moto la Mikocheni, Mch. Dkt. Getrude Rwakatare akitoa Roho Mt. ndani ya Mkoba wake na akiwaambia watu pokea, pokea 'na watu walionyesha kubarikiwa sana'.

[62] Tabia hizi nitazieleza ndani ya andiko hili.

wengi hapa kwetu Afrika[63] na kwa hiyo Tanzania. Lakini pia wakati ule ule tunakubali kuwa mafundisho haya yamekubalika hapa kwetu kwa sababu yanachanganya ufahamu wa Kiafrika kuhusu dunia inayotuzunguka na imani zilizoko ndani yake. Hivyo huchukua Biblia, imani za asili, na ufahamu wa Kiafrika kuhusu ulimwengu unaowazunguka, na mawazo ya kileo kwa umakini sana kwani wanaamini Imani kwa Kristo leo inayajumlisha haya yote kama ukweli alio nao Mtanzania. Na hivyo Mtanzania ili aishi maisha ya uzima tele ndani ya Yesu ni budi aponywe kimwili na kimali ambayo ni alama ya kubarikiwa kutoka kwa Mungu[64]. Hivyo makundi haya yanafundisha Utajiri wa Kifedha na Kiafya.

**Kifedha**

Mafundisho haya kwenye makundi ndani ya Kanisa letu yalianza miaka ya 2000 na kuendelea hadi leo. Kwa mawazo haya, makanisa haya yanafundisha kuwa ukimwamini Yesu na ukaamini ahadi zake basi utabarikiwa na kukua kiroho na kimwili (afya) na utatajirika. Mafundisho haya pia hukaza kuwa umaskini si mapenzi ya Mungu bali ni alama ya dhambi ama kukosa Imani. Wanakaza mafundisho toka (Kumb. 28: 30), pale Bwana alipowaambia wana Israeli wachague uzima ili baraka zote ziwe juu yao (Kumb. 28: 3 - 13). Hivyo utajiri wa fedha na afya njema pia ulitolewa na Mungu mwenyewe wakati wa kutupatanisha, mafundisho yao hunukuu (2Kor 8: 9) na (3Yoh. 2). Ili kutajirika,mafundisho haya hukaza kuwa watu wanahitaji kupanda mbegu ya kutosha yaani kutoa sadaka kubwa ili baada ya maombezi waje wavune mavuno makubwa ama mengi.

Lakini pia leo, miaka hii ya 2010 na kuendelea wameongeza pia mafundisho mengine ya Bwana Yesu kutoa dabo yaani mara mbili ama zaidi tunapomuomba. Mistari kama Marko 10:30b pale Bwana Yesu aliposema wale wanaonifuata watapata mara mia, ama Mathayo15:34 pale Bwana Yesu alipowalisha watu 500 kwa mikate mitatu na samaki wawili. Na mafundisho ndani ya haya ni kuwa Yesu hawezi kukupa kitu kimoja wakati unahitaji viwili. Mfano hawezi toa gari moja wakati unahitaji wewe moja na mwenzi wako moja ili nyote mfike kazini kwa wakati ama mmoja afanye jambo moja wakati mwingine akifanya lingine. Na ili upate dabo inabidi ujihusishe na kazi zinazomtukuza Mungu na kuweka agano na Mungu kuhusu kutoa fungu la kumi kwa mtumishi. Hapa wanachukua maneno haya: Mwanzo 28: 20 -22 Yakobo alipokuwa Bethel na Kumb. 8:17-18, IWafalme 17: 7-16, juu ya Eliya na mjane wa Serepta. Na hasa hii inatumika sana kwani wanaona unahakikisha hata kwa maskini kama yule mjane, Mungu anapenda utoe kitu ili aweze kukubariki mara dufu. Wimbo wa wenzetu toka Afrika Magharibi umepata umaarufu hata kwetu: “Lord is good and gives double, double.”

[63] Kwa uhakikisho wa haya soma, J. Kwabena Asamoah-Gyadu, *African Charismatics: Current Developments,* (Leiden: Koinjeik: 2005),203nk;David Maxwell, *African Gifts of the Spirit,* (Ohio: OhionUniversity Press,2006),204 Faith K. Lugazia: “, “Empires export of Prosperity Theology: Its impact on Africa” in Karen. L. Bloomquist (ed.), *Being the Church in the Midst of the Empire. The Trinitarian Reflections. (*Minneapolis:Lutheran University Press, 2007), 181; Paul Gifford, *.African Christianity. Its Public Role.* (London: Hurst and Company, 1998) 322ff, Ogbu Kalu, "Sankofa”: Pentecostalism and African Cultural Heritage" in *Spirit in the World: Emerging Pentecostal Theologies in Global Contexts,* (Templeton Foundation, 2007), 2.

[64] Lugazia, “ The Gospel’s Promises of Fullness of Life and Critical Considerations of the Prosperity Gospel” Paper presented at sith Theological Workshop, AACC-Nairobi, August,2015..

Tatizo hakuna nafasi ya mafundisho juu ya fungu la kumi kuwa lilitolewa kwa makuhani, Walawi, maskini, yatima na wageni (Kumb 26:12, nk). Maswali kama hivi pesa ninayotoa inahusianaje na baraka za mungu kwetu? Ama Kama ninaweza kumfanya Mungu anitendee lolote kwa kumpa fedha ni Mungu wa aina gani huyo? Mungu anatenda kutokana na upendo, neema na rehema zake zisizo na masharti na wala hatendi kwa kuitikia matendo yetu. Upendo wa Mungu ni kwa wote (Yohana 3: 16). Baba Askofu Ambele Mwaipopo katika hili anasema haya, hata makaka na dada zetu wa zamani akina Abraham na Sarah (Mwanzo 14:18) Yakobo na Rebeka (Mwanzo 28: 10 - 22), Musa na wana wa Israeli (Kutoka 35: 4 hadi Kutoka 36: 7) na hata Daudi (1Mambo ya Nyakati 29: 6 - 16), walikuwa hawatoi ili Mungu awatendee ila walitoa maana waliheshimu nguvu ya Mungu waliyoiona ikitenda kazi katika matukio muhimu katika maisha na huduma yao. Hawakutoa sadaka ili wapate zaidi bali walitoa kwa sababu walijua kuwa Mungu tayari alishawabariki[65].

Urithi wetu wa Kilutheri, katika hili unatukumbusha kuwa "matendo yote ya upendo na hata sadaka tufanyayo/ tutoazo si kwa ajili ya kutufanya sisi kuwa wema ama kuwa karibu zaidi na Mungu, Luther anasema, tunafanya hivyo kama itikio la kukubali wema na upendo wa Mungu kwetu. Kwani kwa kubatizwa, tayari tuko karibu na Mungu na ni Neema yake tu inayotufunika na inayotuwezesha kusimama mbele za Mungu.

**Utajiri wa Kiafya - Uponyaji**

Utajiri wa afya pia unakazwa katika vikundi hivi kuwa Kristo anapotuokoa anataka tuwe wazima wa afya. Kristo alituondoa katika laana ya sheria (Gal 3:13) na laana hii huhesabika kama magonjwa, mapepo, mizimu ya mababu, vifo na umaskini.[66] Mstari wanaokaza sana ni ule wa (Isaya 53:5) kwa kupigwa kwake sisi tumepona.(sala na maombi yao hujikita katika maneno haya) Hivyo Kristo anaponya magonjwa yote. Hivyo wanakaza sana maombezi hasa kwa wagonjwa. Maombezi haya hufanywa kwa kufunga kwa wale walio na Karama. Muda wa kufunga unategemea mwombaji. Ila wote hufikiri kuwa kufunga kwa muda mrefu ndiko kunajibiwa haraka. Wengi wao wanapoumwa hawaendi hospitali bali hukaza kubaki katika maombi. Lakini kuna wale wanaoona kuwa yote yanaweza kufanyika na kuna wanaokataa kwenda hospitali.

Kuhusu uponyaji niseme Walutheri walio wengi hasa hawajiungi na makundi haya kwa ajili ya kuwa matajiri wa mali. Wengi wao wanatafuta uponyaji wa magonjwa sugu yanayosumbua nafsi zao. Mwana elimu jamii na elimu juu ya watu E. M. Uka anasema: "…kwa jinsi waafrika walivyo, mara zote hutafuta nguvu za asili kuwasaidia ama kuingilia kati katika mambo yao yote."[67] Ndiyo maana hadi leo tunakuwa na ndugu zetu wengi ama hata miongoni mwetu magonjwa mengi yanafikirika kuwa yanatoka kwa roho chafu, watu wanaotunenea mabaya, wabaya wanaotuonea wivu kwa afya, elimu na hata yale tuliyonayo ya maendeleo.[68]

---

[65] Ambele Mwaipopo, *"*Maana ya utoaji wa Kikristo na Aina za utoaji *" katika Umoja na Utambulisho Wetu: Mkusanyiko wa Mafundisho ya Msingi Kuhusu Umoja na Utambulisho wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania*, (Moshi: Moshi Lutheran Printing Press, 2013), 118 - 137

[66] Jerry, Savelle, *Prosperity of the Soul* (Tulsa: Harrison House, 1979), 54.

[67] E. M. Uka, (ed.), *Reading in African Traditional Religion: Structure, Meaning, Relevance, Future* (New York: Peter Lang, 1991), 34.

[68] Hebu tukumbuke sote pale tunapokuwa na huduma ya kushauri ama kutunza kichungaji, maelezo ya wateja wetu si huwa yamejaa maelezo ya jinsi hiyo?

Mawazo haya hayana utofauti na mawazo ya kale katika jamii yetu. Mtu alipokuwa mgonjwa iliaminika kuwa ama mizimu au watu wabaya (hawa waweza kuwa ndugu wa karibu ama mbali, marafiki zetu, n.k), (wachawi) wamesababisha ugonjwa. Ili uponyaji utokee basi sala zilitolewa kwa mababu ili aliyeugua aponywe/ ama shida ilipogundulika kuwa kubwa zaidi basi damu ya mnyama ilitolewa kama sadaka ili mgonjwa ambaye pia aliaminika ametenda dhambi asafishwe.

Makundi haya katika magonjwa yanaamini kabisa kuwa magonjwa yanatoka katika nguvu hizo nilizotaja awali/ ama dhambi ya mgonjwa ila, sala zinaelekezwa sana katika **jina** ama **damu ya Yesu**. Sala hizo zinaweza kuongezewa ama kuguswa ama kuwekewa mikono/ kubarikiwa au kupakwa mafuta (Yak. 5:14). Miaka hii 2000 na kuendelea, tumeshuhudia tena alama nyingine **za mazao ya Israeli kama mafuta ya mizeituni, maji ya Yordani na hata mchanga kutoka Israeli kuwa yanaleta baraka na yanakuondolea mikosi.** Maombi na maombezi kwa ajili ya uponyaji (‘healing’ na siyo ‘curing’) na kujikinga na nguvu za giza ni moja ya tendo la kiimani linalochukua nafasi kubwa katika liturgia ya makundi haya. Hivyo basi kuokoka kwao si kuzaliwa mara ya pili tu ama kusafishwa dhambi na kuingizwa katika Ufalme wa Mungu bali pia ni kukombolewa kutoka nguvu na mamlaka za giza za dunia hii ambapo magonjwa vifo na umaskini vinachukua nafasi kubwa. Kwa mwenye mapepo wanafanya kama Kristo alivyofanya (Marko 5: 8), nk.

Kama wao hata nami, naamini nguvu za ajabu zipo (yaani miujiza). **Nionavyo mimi sisi Wachungaji tunahitaji kutofautiana na wenzetu kwa kuwa jasiri kueleza chimbuko la ugonjwa/ matatizo, pia tusitumie njia moja ya sala za uponyaji. Tuangalie hata Bwana Yesu alipoponya kipofu alitumia mate. Kiwete alitumia maji ya kwenye birika na mwingine alitumia tu maneno**. Badala ya Kanisa letu kusema haya hayapo, nadhani sasa ni wakati tuwaambie watu wetu ukweli kuwa kwa vile Mungu ni juu ya ufahamu na utendaji wetu, kuna mambo yanayotujia ambapo sisi hatuna majibu kamili ila hakika Mungu wa Utatu ndiye ajuaye. Hivyo kwanza tuanze kufanya ushauri kichungaji, ili tujue ama kusikia kuwa tatizo tulifikishe wapi. Kama ni hospitali, tuwaelekeze watu kupata utaalamu wa walio na vipawa kule hospitalini lakini kama tatizo si la hospitali wachungaji tuwaombee. Na mtu asipopona, tusijisikie vibaya ama kujiona kuwa hatuna Imani au upako.

**Unabii na Maono**

Kwa kutumia hofu inayotokana na ufahamu wetu kama Waafrika na matatizo yaliyoko tayari ndani ya jamii yetu hapa nchini, makundi haya wakati mwingine yamegeuza watu wema kuwa wabaya kwa sababu zisizo za kweli. Ninasema wanachanganya ufahamu wa Kiafrika maana wenzetu wazungu wanapopatwa na shida na haswa ya ugonjwa, mara zote hujiuliza swali la “Hivi shida hii imesababishwa na nini?” Na sisi Waafrika swali letu wakati wa shida huwa: “Hivi shida hii imesababishwa na nani?” Hivyo kabla ya maombezi hasa kwa wagonjwa, na wenye shida mbalimbali ndani ya jamii mfano kukosa mtoto, kufiwa mara kwa mara, kukosa mchumba ama kuachwa na wachumba mara kwa mara, watoto kufeli katika masomo na magonjwa kama UKIMWI, ama ya kichwa kama kichaa, ama kifafa; wana maono hufunga na kuomba kuuliza shida ya muumini imesababishwa na nani?

Basi waonaji huona aliyesababisha shida. Kundi hili ni hatari sana, kwani kwa kutumia mbinu hiyo ya mtazamo wa Kiafrika, ndugu zetu wengi hata wengine yawezekana wakawa ndani ya mkutano/ ama baraza hili wamelikumbatia sana. Huelekeza sala za kuomba kwa kufunga na

kukesha wakitafuta mbaya. Mara nyingi mbaya amekuwa jamaa wa karibu na mwenye shida ama hata ndugu wa karibu. Katika hili, makundi ya uamsho wa kikarismatiki ndani ya Kanisa letu wamejikuta katika matatizo makubwa ya kimahusiano ndani ya familia.

Mafundisho ya jinsi hii, badala ya kumuonyesha Yesu wa Upendo na upatanisho yamemuonyesha Yesu kuwa ni mleta uadui. Hivyo unakuta ndugu wameokoka na wote wako katika maombi ila hawasalimiani na hawana ushirika wa pamoja kwa madai ya kutendeana maovu. Ndiyo maana moja ya sababu waumini wengine hawajaitikia uamsho huu ni kuwa wanajiuliza kama wokovu ni kufahamu wakristo wanavyotenda uovu ama kuchukiana kuna sababu gani ya kutafuta wokovu huu?

Ni kweli Roho Mtakatifu anatoa karama hizo wanazotafuta. Lakini upotofu unakuja pale: Kwanza, wanapopunguza karama za Roho Mtakatifu na kutaja nne tu. Roho Mtakatifu anapokuja kwetu kama zawadi hutoa karama mbalimbali kwetu. Ukisoma 1Kor 12-14; Rumi 12:6-8; Efeso 4:11 na 1Petro4:9-11 vifungu hivi vinazungumza juu ya karama atoazo Roho Mtakatifu. Lakini mimi ninapenda kuongeza kuwa hizi ni baadhi tu ya karama si jumlisho ya Karama zote atoazo Roho Mtakatifu. Kuna karama nyingi zaidi ambazo si rahisi kuorodhesha.

Kwa habari ya wingi wa karama na utendaji wetu kwa kuwa na karama hizo hilo limekuwa swali kwa waumini na kuleta changamoto miongoni mwetu. Niseme mwenzako akiwa na kitu kizuri nawe una uwezo wa kukipata ni vizuri kujifunza lakini niseme kwa habari ya karama za Roho Mtakatifu ni Yeye Roho atoaye si Kanisa wala mtu fulani hivyo basi, ni muhimu sana tumuombe huyu Roho Mtakatifu badala ya kutafuta njia ya mkato kwa kuiga watu wengine.

Shida ya Pili, ni pale karama za Roho Mtakatifu zinapowekwa katika makundi ya Karama kubwa na ndogo. Na kuwa wenye hizo ndiyo wako karibu na Yesu kuliko wengine.

Shida ya Tatu, ni pale wanapotumia karama za Roho Mtakatifu kwa kujijenga badala ya kulijenga Kanisa. Wengi wenye karama za Uponyaji, hujitahidi sana kuonyesha kazi yao ili wawapate waumini. Pia wenye tatizo hufikiri kuwa mwombaji ndiyo yuko karibu na Yesu na hivyo humng'ang'ania huyo. Baada ya muda akijitokeza mwingine, watu wanahama, nk.

Nne, pale wanapofanya watu waamini kwamba wanaweza kuwapatia karama yeyote kwa kuwaombea.

**Changamoto Chanya za makundi haya**

Ni muhimu katika sehemu hii nianze kusema kuwa mafundisho ya uamsho wa vikundi vya kikarismatiki vilivyomo ndani ya Kanisa yanaleta changamoto kwenye muundo mzima wa kanisa letu. Changamoto zinazosababishwa na watu kuiga mafundisho pasipo kufahamu kwa kina (Copy and Paste). Lakini pia changamoto ya Ukosefu wa Kinga ya Kiroho (Ukwakikiro)[69]. Elom Dovlo anasema Changamoto ni hatua ya kujikosoa kutokana na matukio mengine. Katika kujikosoa huku mmoja anahitaji kuweka mbali ujuaji wake, udhuru ama visababisho

[69] Ukosefu wa Kinga Kiroho, (Tumekuwa na masomo ya Biblia kwenye Kanisa letu [Sharika], yasiyo na malengo ya kukidhi hitaji bali kutimiza utaratibu wa ripoti zetu).

visivyoridhisha ili tuelewe na kuitikia wito unaojenga utamaduni wetu.[70] Hivyo kwake changamoto ni ulazima wa kujikosoa kwa kuangalia uwezo na madhaifu yanayotokana na ufahamu wetu.[71]

Mlahagwa, kwa upande wa Tanzania anasema: "Changamoto ya madhehebu hayo/ ama makundi haya kwa kanisa letu ni kuwa watu wameongeza kusoma Biblia na kuwa na kiu ya kulifahamu Neno la Mungu na pia namba ya waumini wa Kikristo imeongezeka. Vikundi vya maombi vimeimarika na Wakristo wengi wameweza kuomba kwa maneno yao. Watu wamefumbuliwa macho kutumia zaidi vipawa vyao kama kufanya maombezi kwa wagonjwa na maombi kwa wenye shida mbalimbali. Hakika watu wengi waliojiunga na makundi wamebadilika kimaadili."[72]

Vikundi hivi vimesukuma kasi ya ushirikishwaji wa wanaume, wanawake na vijana katika Kanisa letu kuliko vigezo vingi vinavyotumika ndani ya kanisa kushirikisha jinsi na marika mbalimbali ndani ya kanisa. Vikundi hivi pia vimesukuma dhana ya umoja ndani ya Kanisa letu lakini pia na madhehebu mengine kama ndoto za umoja wa makanisa ya Kilutheri duniani zinavyoshauri." Mbali na haya yote watu wameponywa miili na roho kupitia makundi haya. Mwana uamsho wa kikarismatiki anaposema ana amani anaionyesha kuanzia katika uso wake.

**KANISA LETU TUFANYE AMA TUKAZIE MAHALI GANI (*Eccleia Semper Reformanda yetu)* TUNAPOLETA UAMSHO BAADA YA MIAKA 500 YA MATENGENEZO?**

Ninapoingia katika sehemu hii ambayo ni sehemu elekezi, ninapenda nianze kwa kukumbusha kuwa Mungu wetu wa Utatu ametumia njia mbalimbali kuliamsha Kanisa lake. Mungu hakutumia tu njia ambazo labda wanadamu tungependa ama hata wakati mwingine ametumia njia ambazo tusingezifikiria katika vipaumbele katika kuleta uamsho.

Karne za Mwanzo, Mungu alimtumia kiongozi wa kisiasa, Mfalme Constantine, kiongozi ambaye wala hakuwa Mkristo akamhekimisha kwa Roho wake Mtakatifu. Mfalme huyu kwanza akaruhusu Ukristo kuwa dini ya himaya na kuzuia kabisa mateso kwa wakristo. Mfalme aliwaita viongozi wote wa kanisa la Kristo ili wajadili jinsi ya kuliamsha Kanisa. Ingawa malumbano yalichukua muda mrefu, hatimaye amani na uamsho vilipatikana.

Wakati wa Matengenezo, Luther hakufanya kama Mfalme Constantine, la! Badala yake aliketi kwanza akaandika maandiko mengi tu, na "Kairos ya Bwana" ilipofika alieneda kuwasilisha maandiko yake kwa wahusika na ndipo sasa akaanza kujadili jinsi anavyoliona Kanisa kupoa kwake na jinsi anavyofikiri Kanisa lifanye ili liamke. Bahati mbaya njia yake (method) haikukubaliwa mara moja na akatengwa.

Kanisa letu kwa mtazamo wangu limekuwa katika kufuata nyayo za Martin Luther katika kuliamsha Kanisa. Hebu nikumbushe kuwa Mkutano wa Wachungaji Januari, 1997 pale Kigurunyembe, Morogoro ulijadili uamsho ndani ya Kanisa kwa kina. Baada ya kuangalia

[70] Elom Dovlo, "A Comperative Overview of Independent Churches and Charismatic Ministries in Ghana" in *Trinity Journal of Church and theology,* 2,2(1992)62

[71] Ibid.

[72] Mlahagwa, *Contending for the Faith 296-297*

upungufu uliyopo, ndipo ilikubalika kuwa sasa Wachungaji tuanze kuwa na mikutano ya uamsho na vikundi vya maombi ndani ya Kanisa letu.[73] Zoezi hili lilikuwa endelevu kwani Wachungaji tumefanya hili na kwa wale walio na mipango na malengo wamelipa jambo hili kipaumbele.

Mwaka 2012-2013, Kanisa letu kupitia Kamisheni ya Theolojia na Maadili (KATHEMA), lilionelea haja na wajibu wa kuweka yaliyomo ya mafundisho yetu katika maandiko, ili tunaposema kufundisha, tuone hasa tunafundisha nini. Haya yaliyomo yalitokana na jinsi kanisa linavyoona upotoshwaji wa urithi wetu ndani ya makanisa yetu. Yalichukua mambo muhimu ambayo Kanisa letu linalaumiwa kwa kutoyaelekeza kwa waumini wetu[74].Wachungaji waliombwa kuyaandika kwa umakini kama watheolojia wa kilutheri. Yaliyomo yake yako ndani ya Kitabu kiitwacho: "*Umoja na Utambulisho Wetu: Mkusanyiko wa Mafundisho ya Msingi Kuhusu Umoja na Utambulisho wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania*. Moshi: Moshi Lutheran Printing Press, 2013". Pale makumira wakati wa jubilii ya miaka 50 tangu kuundwa kwa Kanisa letu la Kiinjili Kilutheri Tanzania jambo hili liligusiwa tena na kuombwa kwa pamoja tukafundishe na kuwaamsha waumini wetu. Hili nalo ni endelevu.[75]

Hivyo nilichokuwa nikifanya katika vipindi viwili vilivyotangulia ni kutaka tujifanyie tathmini ya kuwa haya tuliyokubaliana tumeyafikisha wapi? Je tumeonaje mwitikio wake na tuchukue hatua ipi zaidi kuleta ama kuendeleza uamsho na hasa wakati huu tunapoingia mwaka wa 500?

**Hapa ninaomba niseme mambo mawili**
Ninaamini uamsho wa kweli na unaolijenga kanisa ni ule unaotaka sisi watumishi tushuhudie lile tunalolijua na kuliamini. Kwa hiyo matenengezo ya Kanisa leo yasichukuliwe kama tu ni kule kuelewa matukio yaliyotokea wakati fulani bali tuyatafsiri katika wakati na mahitaji yetu leo. Kuchagua mafundisho fulani kuwa muhimu na mengi si muhimu kamwe; kutaendelea kuligawa kanisa letu badala ya kulijenga. Pendekezo hapa ni kwamba tukaze mafundisho ya Biblia na Urithi - Doctrine zetu/kiri zetu. Pili, tuwe na senta za kiroho.

**Tukaze mafundisho ya Biblia na Urithi-Doctrine zetu/kiri zetu**
David G. Truemper anasema, "Ingawa Walutheri tumekiri kuwa kiri (Confessions) zinaungamanishwa katika katiba na miongozo ya Kanisa letu hatujawahi kuweka bayana hizo kiri zitatumikaje kama mafundisho ya msingi kwa kanisa."[76]. Nikianzia kwetu Wachungaji, Kiri tunazofahamu ni Imani ya Mitume tu. Wengi wetu kuanzia Imani ya Nikea na hasa Athanazio-hatujakutana nazo popote. Hata pale tulipokutana nazo tunalofahamu ni kuwa imani hizo ni kwa ajili ya sikukuu za kanisa lakini hatuna historia wala maana ya Kiri hizo na jinsi tunavyoweza kuzitumia kama jibu la maswali ndani ya jamii hasa kwa wakati wetu.

[73] Aligawesa,Mkutano Mkuu akimueleza Mlahagwa.,298
[74] Manase E. Mzengi, "Lutheran Understanding of the Role of the Holy Spirit and Challenges from Pentecostal Churches in the ELCT Central Diocese" ( BD Thesis, Makumira University College, July 2003), 10
[75] Askofu E. Buberwa katika Mkutano Mkuu pamoja na baraza la wachungaji, ametueelekeza sana juu ya Kitabu hicho.
[76] David G. Truemper, "The Lutheran Confessional Writings and the Future of the Lutheran theology" in .*The Gift of Grace: The Future of the Lutheran theology.* Niels Henrik Gregersen, Bo Holm, et.al. (Minneapolis:Fortress Press,1999),131-144.

Imani ya Nikea kwa mfano inakaza sana mafundisho kuhusu Roho Mt. na Utatu, lakini katika "TEMBEA NA KRISTO", kwa mfano, mafundisho haya yako kwenye Appendix. Hapa pia ninawasihi tupige hatua moja mbele kutoka kwa mafafanuzi ya Martin Luther, kuhusu kazi za Roho Mtakatifu kwani katika Ketekisimo ndogo anasema: Kazi ya Roho Mtakatifu ni kutuwezesha kuamini.[77] Tunajua kuwa Roho Mtakatifu kama (Paraclete) msaidizi, anatuwezesha kusimama imara katika kushuhudia Ukweli wa Kristo, kuimarika katika mateso na majaribu na pia kutukumbusha Kristo aliyofundisha. (Yohana 14: 26) kwa sababu duniani kuna mateso na majaribu mengi kwa waaminio Kristo (Yohana 14). na pia anatoa karama mbalimbali (I Kor 12 - 14), anatuombea (Rum. 8:26), na mengine. Kitabu cha Tembea na Kristo, ni sisi Wachungaji tulitengeneza mafundisho haya. Kwa kuwa fundisho la Roho Mtakatifu ni swali kwenye Kanisa letu leo. Je si ni hekima tukaandaa na kuweka mafundisho ya Roho Mt. ndani ya kitabu hicho? Ninaamini tukiweka mafundisho ya Roho Mtakatifu vizuri yatasaidia wale wanaofundisha vijana wetu wa kipaimara.

Sambamba na mafundisho, tunaourithi mkubwa unaongelea faida za matendo mema kwa muumini. Mfano Ungamo la Augusburg linakaza kuwa, baada ya kubatizwa, tunahitaji kubadilisha maisha yetu na hasa katika kuikataa na kuichukia dhambi kwani hayo ndiyo matunda ya toba (Math 3: 8).[78]Imani ya Athanasio inakaza sana kuwa waliookolewa, kwa njia ya kubatizwa wanahitaji kufanya matendo mema ili waingie katika uzima wa milele.[79] Na mafafanuzi yake yanaweza kwenda kuwa Roho Mt. anatuwezesha kuamini na hivyo kama waumini tunahitaji itikio - Kutenda mema na kukataa mabaya.

Na pia kuwa wokovu ni (process) mchakato. Yaani hatuwezi kusema niliokoka siku ile nilipobatizwa. Bali tunaokolewa kila siku. Hivyo kukaa katika Neno na kulitenda ni fundisho la Bwana Yesu. Hapa ninashauri, ndani ya jumuia zetu pamoja na mafundisho mema tunayoandaa, tuweke mafundisho yaliyoko katika kiri na maungamo yetu na hasa tukikazia maadili mema kwetu watumishi na kwa muumini wa kanisa letu. Kwa vile kitabu chetu cha TMW kina sehemu kubwa ya mafundisho haya basi nacho kitumiwe katika jumuia zetu.

Katika kufundisha urithi wetu tusibaki tu kuomba radhi (apologetic) kwa kufundisha yale tunayopenda ila tuseme ukweli wa yaliyomo yote. Mfano katika TMW, mafafanuzi ya Sala ya Bwana ambayo tumetumia leo yako kutoka katika Katekismo ndogo. Na yanapo fundisha "utuepushe na mwovu", yanaongelea maneno rahisi kwa sababu iliandaliwa iwafundishe watoto ndani ya familia. Lakini kubwa, inasema kuwa, "Mwovu tunayeomba kuepushiwa ni: mikosi yote na yote iliyoko katika utawala wa mwovu kama: Umaskini, aibu, kifo, mikosi yote itokeayo duniani. Kwani mwovu analeta hata ajali.[80]

Kama tunafuata urithi wetu, mpendwa mwana uamsho wa Kikarismatiki anapoomba kwa ajili ya kuondoa mikosi, mabalaa umaskini na hata mapepo amekosea nini katika urithi wetu? Anaposema tuache wizi na uzinzi, kiburi kusengenya kwa mtazamo wa Biblia na ungamo la Athanasio ana kosa gani? Ninataka kusema pia kuwa badala ya kufikiri kuwa waumini wetu

[77] Martin Luther, *Katekismo Ndogo.TMW*-688
[78] M. Luther, *Augusburg Confession - Article XIII. In BC:35*
[79] *Tumwabudu Mungu wetu,*681
[80] Martin Luther, *Large Katechism in The Book of Concord: The Confessions of the Lutheran Church, (*Theodore G. Tappert-Ed. (Philadelphia: Fortress Press, 1959). 435.

wanaiga kwa wengine, tuangalie vema jinsi ya kufundisha mambo haya ambayo ni maswali kwao ambapo mimi ninaona kuwa wametangulia vyuo vyetu vya theolojia katika kutoa mafafanuzi elekezi ya kiri zetu. Na haya pia yaingizwe katika mtaala wa mafundisho ya Jumuia.

Mafundisho mapya ambayo, nionavyo mimi ni ya kuigwa na haya inabidi sisi Wachungaji kwanza tuyafahamu na kukubaliana hapa kupitia vyuo vyetu vya theolojia ni haya:

Injili hii ya Utajiri ( Prosperity theology)
Utajiri wa Kimwili na kiroho kukazwa kuwa utajiri wa kimwili na wa mali tu. **Kanisa** letu limekumbatia vizuri mafundisho haya kupitia vikundi vya Uamsho wa Kikarismatiki. Nami ninafikiri ni mafundisho mazuri kwani Kanisa tunahitaji kupata fedha ili likue na kuendelea. Hata wana matengenezo walikubali kuwa mtu binafsi ama kanisa kuwa na mali ni jambo jema[81]. Lakini shida ya mafundisho haya kwa sasa iko katika watu kuambiwa kuwa wasipotajirika ama kupona ni kwa sababu ama hawajaomba sawasawa, hawajapanda mbegu ya kutosha ama wameweka kidogo sadaka yao kwenye bahasha ya ukombozi, ama bado wana dhambi.

Tunapo hamasisha mavuno kwa mfano, ama harambee, ni mara chache sana tusiposikia sentensi hizi: "Usipotoa Bwana hatakubariki, Bwana hapendi Mkono wa Birika. Ama ukiwa bahili Bwana atachoma mazao yako," nk. Magonjwa na adha nyingine yanahesabika kama dhambi ama nguvu za giza hata wakati mwingine waumini wanaaminishwa kuwa yanatoka ndani ya familia. Sasa tumekwisha anza habari za fungu la kumi na makanisa mengine (kilutheri) yanafanya fungu la kumi ni kwa Mchungaji.[82] Sisi wenye kanisa la muundo tangu chini hadi juu tukiendeleza hayo si itakuwa vita?

Ninafikiri kwetu ni muhimu sana tukakaza na utajiri wa kiroho pia ambao unamsaidia Mkristo kuelewa kuwa maisha ya Mkristo yanategemea mapenzi ya Mungu na wala si matashi ya mwanadamu. Kumsaidia Mkristo kujua kuwa hata sehemu ya mateso, magonjwa, umaskini na maradhi ni sehemu ya uumbaji wa Mungu na wala si mapungufu ya muumini au dhambi yeyote, kwani wapo wakristo miongoni mwetu ambao ni wacha Mungu kama sisi lakini hawajafanikiwa kuwa na watoto na hospitali wamedhihirishiwa kila mara kuwa hakuna mwenye tatizo.

Wapo waumini ambao wana watoto watatu na wote ni vilema ama vichaa. Na wapo walio na watoto waliopata ugonjwa tangu wazaliwe na kuna uwezekano wa kufa wakiwa bado na hayo magonjwa. Ninataka kusema, ni muhimu kuwaonyesha ama kuwafundisha ndugu zetu waumini kuwa Imani kwa Kristo si ya upande mmoja wa sarafu bali lazima iwe na pande zote mbili. Na hapo inakuwa imekamilika. zaidi ya kuelekeza kimwili tu. Si hilo tu, bali pia tusitake kukamua maziwa kutoka pundamilia. Wale wasionacho tuwaheshimu badala ya kuwanyang'anya hata hicho kidogo walichonacho.[83]

[81] Martin Luther, *BC Apology of the Augusburg Confession, 224.*
[82] Ambele Mwaipopo, "Maana ya Utoaji …"
[83] Faith K. Lugazia, "Empires export of Prosperity Theology: Its impact on Africa" in Karen. L. Bloomquist. Ed. 2007 *Being the Church in the Midst of the Empire. The Trinitarian Reflections (Minneapolis*: Lutheran University Press) 181-191

**Mafundisho ya unabii na maono** vinahitaji kukemewa hasa.
Hii ni kwa sababu nionavyo mimi, watu wetu wengi wamekwama hapa kiimani. Wakristo wameaminishwa kuwa maono na unabii vina msaada kwa muumini kutambua chimbuko la tatizo. Hali hii imeleta uhasama sana ndani ya watu wa Mungu. Tuwafundishe watu kuwa magonjwa, ugumba, kichaa na mengine yalikuwepo tangu mwanzo na yataendelea kuwepo ili utukufu wa Bwana udhihirike (Yohana 9:3).

Lakini pia tuwafundishe kuondoa hofu kwa kuwakumbusha wajibu wao wa kuomba. Matatizo yakiwapata wahesabu kuwa kama jaribu na kuomba ili jaribu liondoke badala ya kuamua kuhamia kwa waombaji. Ama kuanza kujiuliza maswali yenye kuelekeza sababisho. Hapa ninaomba tuone haja ya kupanua wigo kuhusu huduma ya maombi. Tusifikiri kuwa na sala zilizoko katika Liturgia tu bali tuombe sala zinazoelekeza jibu kwa swali la muumini na kukaza kuomba mapenzi ya Mungu. Tukumbuke kuwa tumeitwa kulisha na kuchunga kondoo (Yoh 21: 15 - 17). Na hata kutopoteza hata mmoja,(Yoh.17:12).

**Kuhusu Vipawa vya Roho Mtakatifu**, tufundishe kuwa ni vingi si tu (Kunena kwa Lugha, Unabii, maombezi na miujiza). Wale waombao na hata kunena kwa lugha wanathaminiwa kuliko wale wenye vipawa vingine kama kufundisha na hata kulea. Kanisa letu tuwasaidie watu kuwaelimisha na katika hili pia, turuhusu baadhi ya mambo ambayo hatufanyi, kutendeka ndani ya Kanisa letu. Mfano Kunena kwa Lugha. Mtume Paulo hakukataza kunena kwa lugha ila alisema, aombe pia kupata ufasiri (1Kor 14:13), na afanye kwa utaratibu "…msizuie kunena kwa lugha" (1Kor.14:39;b). Hapa nina maana tusionyeshe kuwa kitu hicho hakipo bali kinaweza kufanyika na kuwa hakimfanyi mtu kuwa mkristo zaidi ya wengine. Na muhimu zaidi tuseme kuwa karama ni kwa ajili ya kulijenga kanisa la Kristo na si kumjenga mtu binafsi. Hivyo kama kuna mtu mfano ana karama ya Lugha ngeni basi itumike ndani ya Kanisa na ile ya Lugha binafsi aitumie pengine si wakati wa Ibada.

**Mafundisho ya maana za Sakramenti**
Tukazie mafundisho ya maana za Sakramenti katika vipindi vya Ubatizo, Kipaimara na hata katika jumuia ndogo ndogo. Waumini wetu wengi leo, wamefanya ubatizo kuwa ni habari ya sherehe zaidi ya sakramenti. Nashauri ikiwezekana baadhi ya siku tukumbushe mambo hayo kwa waumini si wale wenye kubatiza na kudhamini tu. Mfano kuhusu ubatizo tukaze habari za kuwa Sakramenti zaidi ya kukaza kuwa Ubatizo wa aina fulani ndiyo unatenda mambo fulani.

**Tuwe na Vituo vya Senta za Kiroho**
Ninadhani sasa wakati umefika ambapo Kanisa letu kwa ukubwa wake linahitaji kuwa na vituo vya kuwajenga na kuwaganga watu waliovunjika moyo. Waheshimiwa watumishi wa Mungu, ninashauri kuwa kanisa liingie gharama kwa kuanzisha vituo ya umoja vya senta za kiroho. Na wale ndugu zetu Wachungaji wenye karama za kikarismatiki tuwape kazi maalumu ya kuhudumu ndani ya vituo hivyo (to act as referral Spiritual healing centres).

**Jumlisho: Tukaze mambo ya maadili yenye ushuhuda**.
Mtazamo wangu kwa ujumla ni huu kuwa Wachungaji tumepunguza kuwa mashahidi wa Kristo katika maisha yetu. Dhamiri zetu zimeshindwa kutushitaki. Tumekosa Upendo kati yetu na ama tumeoneana wivu au kukomoana. Haya kwa mtazamo wangu yanasababisha Kanisa kupoa.

Uamsho wa kweli na wenye kuleta mapinduzi utakuwepo endapo sisi kama watumishi tutakiri kuwa na haja ya kusikia kwa Upya Uwepo wa Kristo katikati yetu. Na kuwa Kristo huyu anatutaka tuyatende mapenzi yake kwa utukufu wake.

Tuombe sana tena kwa Imani. Haya yatokee.

Kristo atubariki.

Naitoa kwa heshima Mjoli mwenzenu: **Mchg. Dkt. Faith K. Lugazia**

Andiko kwa ajili ya Mkutano wa Wachungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), 24 - 29 Septemba, 2016.

## NUKUU:


Baird. Robert. Chandram. Russel. "Report on the Faith and Order Working Committee on the *Church Union Conversation,Limuru Kenya"* Minutes of the Faith and Order Commission, Geneva, 1962,45-46.

Cox. Harvey. *Fire from Heaven: The Rise of Pentecostal Spirituality and the Reshaping of Religion in the 21st Century.*Reading,Maddison-Wesley,1996.

Dowley. Timothy. Ed.*Introduction to the History of Christianity: First Century to the Present Day.*(Minneapolis: Fortress Press,2002.

Gonzalez. Justo L.*The Story of Christianity: The Early Church to the Dawn of the Reformation,*Vol.1.San Fransisco: Harper Collins,1984.

Grenz Stanley J,et,ala.,*The Pocket Dictionary of Theological Terms.* Illinois:Intervarsity Press,1999.

Hotuba ya Mwl. Julius Kambarage Nyerere ya 2November, 1978 pale Diamond Jubille. http://www.jamhurimedia.co.tz/uwezo-wa-kumpiga-tunao-sababu-ya-kumpiga-tunayo/(accessed 15,May,2016)

*"Joint Declaration on the Doctrine of Justification". Pontifical Council for Promoting Christian Unity. 31 October 1999.*( Retrieved 2014-01-17.

Kibirah, Josiah M. "Has Luther Reached Africa: The Testimony of a Confused Lutheran" in ATJ,12:1(1983)6-15

Kibira. Josiah M. *Church, Clan and the World.*( Uppsala: Almquist and Wiksell,1974.
Kabugumila, Simeon. "Conversion and Revival:A Critical Analysis of the Revival Movement among Lutheran Christians in North Western Diocese of the Evangelical Lutheran Church in Tanzania." Unpublished:PhD Dissertation. University of Kwazul Natal, Pietrmaritzburg, 2005.

Laiser, Naaman. "The Communion of God and Man in the Holy Spirit: A Study of the Concept of the Holy Spirit in Contemporary Lutheran Thinking" . Th. D. Diss., Hamburg, 1981.

Lohse Bernhard D. *Martin Luther's theology: Its Historical and Systematic Development.* Minneapolis: Fortress Press, 1999.

Lugakingira. Wilson K. "Kanisa na Umasho: Andiko kwa Mkutano wa Wachungaji Morogoro,1997" Halijachapishwa.

Lugazia. Faith K. "The Relevance of Smalcald Articles in Tanzanian Christianity,Andiko lililosomwa katika mkutano wa Smalkadia,Ujerumani 23,2012.Halijachapwa.

Lugazia. Faith K. "Charismatic Movement and the Evangelical Lutheran Church in Tanzania" in *Charismatic Renewal in Africa: A Challenge for African Christianity.* Mika Vähäkangas and Andrew, Kyomo. Eds.Nairobi: Acton Publishers,2003. 45-65.

Lugazia. Faith K. "The Challenges of Charismatic Movement in the ELCT and the Need for Cooperation." : A Case of the ELCT/Eastern and Coastal Diocese" Master'sThesis.St. Paul Minnesota,2001.

Kijanga. Peter. "Ubatizo na Roho Mtakatifu" in Essential Essays on Theology in Africa, Arusha: Makumira Publications. 5th.Ed. Leonidas Kalugila and Nancy Stephenson, 1987..

Lugazia. Faith K. "Itikio la Changamoto za Vikundi vya Kikarismatiki na Upentekoste kuhusu (Uponyaji na Matendo ya Miujiza) katika Kanisa letu". Andiko nililotoa Makumira, Km itikio kwa mtoa Mada hii. Mch. Dkt. Msafiri Mbilu, Juni, 2013.

Kwabena Asamoah-Gyadu. J. *African Charismatics: Current Developments,* Leiden: Koinjeik: 2005.

Maxwell. David. *African Gifts of the Spirit,* (Ohio: OhionUniversity Press,2006.

Lugazia. Faith K. "Empires export of Prosperity Theology: Its impact on Africa" in Karen. L. Bloomquist. Ed. *Being the Church in the Midst of the Empire.The Trinitarian Reflections.* Minneapolis:Lutheran University Press, 2007. 181-187. Gifford. Paul. .*African Christianity. Its Public Role.* London: Hurst and Company, 1998.

Ogbu Kalu, "Sankofa": Pentecostalism and African Cultural Heritage" in *Spirit in the World: Emerging Pentecostal Theologies in Global Contexts.*Templeton Foundation, 2007.

Lugazia. Faith K. " The Gospel's Promises of Fullness of Life and Critical Considerations of the Prosperity Gospel" Paper presented at sixth Theological Workshop, AACC - Nairobi, August, 2015.

Mwaipopo. Ambele. *"*Maana ya utoaji wa Kikristo na Aina za utoaji *" katika Umoja na Utambulisho Wetu: Mkusanyiko wa Mafundisho ya Msingi Kuhusu Umoja na Utambulisho wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania*, (Moshi: Moshi Lutheran Printing Press, 2013), 118-137

Savelle, Jerry.*Prosperity of the Soul*. Tulsa: Harrison House, 1979.

Luther. Martin. "Lecturers on the Epistle to the Romans" (1515). *Luther's Works, Vol.34. Philadelphia:Fortress;St. Louis: Concordia Publishing House,1955-86.*

uther. Martin. (Law and Gospel" "Injili na sheria",*WA 391,361,1-6*

Mambo .George K. *The Revival fellowship (Brethren ) in Kenya.*Kenyan Churches Handbook, Kisumu.

Mlahagwa. Josiah R. "Contending for the Faith:Spiritual Revival and the Fellowship Church in Tanzania" in *East African Expression of Christianity. Thomas Spear and Isaria Kimambo.* Eds.Dar es salaam: Mkuki na Nyota, 1999.

Munga, Aneth Nyagawa. *Uamsho: A Theological Study of the Proclamation of the Revival Movement with in the Evangelical Lutheran Church in Tanzania*. Lund: Lund University Press.1998.

Mushemba, Samson B. "The History of the Revival Movement in the Evangelical Lutheran Church in Tanzania, Northwestern Diocese." M.Th. Thesis. Luther Northwestern Theological Seminary, 1982.

Mwombeki, Fidon. "Roho Mtakatifu" in *Wakristo Tusemezane.* Morogoro: CCT Idara ya Maandiko. 1988.

Niwagila, Wilson B. *From the Catacomb to the Self-governing Church: A Cases study of the African Initiative and the Participation of the Foreign Missions in the Mission History of the North-Western Diocese of the Evangelical Lutheran Church in Tanzania, 1890-1965.*

Ammersbek b. Hamburg : Verlag an der Lottbek, 1988.

Orr. Edwin J. *Evangelical awakening in Africa.* Minneapolis: Bethany Fellowship,1975.

Packer. J. I. *Revival: Rediscovering the Holiness: Knowing the Fullness of Life with God,2009*

Placher, William. *A History of Christian theology: An Introduction.*Penslyvania: Westminster press, 1983.

Rweyemamu. Josephat. *Convention Discourse in African Perspective.*Kamen: Hartmut Spenner,2014.

Sendoro. Elinaza. *Uamsho na karama: Roho Mtakatifu katika Makanisa ya Kihistoria.*Moshi: Millenium Books,2000.

"Strategic Framework for the Third Medium Term Plan (MTP-111)for the Prevention and Control of HIV/AIDS/STDs 1998-2002" .Ministry of Health: Tanzania Mainland, 1998).

Sundkler, B and Christopher Steed, *A History of the Church in Africa* (Cambridge: Cambridge University Press, 2000), 1012.

Sundkler. Bengt. *Bara bukoba: Church and Community in Tanzania.*London: C.Hutst,1980.
*The Concise Oxford English Dictionary,11th Ed. 2004*

UNAIDS/WHO, "Epidemiological Fact Sheets on HIV/AIDS and STD Infections," Tanzania 2002 Update.

Vahakangas,Mika. " Teaching Lutheran Theology in Tanzania-On the (Ir)Relevance of Lutheran Theology, in *Dialog: A Joournal of Theology.* Vol.42.(2),2008, 171-174

Welbourn. F. *East Africa Rebels.*London: Oxford University Press,1962.

Uka.E. M Ed. *Reading in African Traditional Religion: Structure, Meaning, Relevance, Future.* New York: Peter Lang, 1991.

Dovlo. Dovlo. "A Comperative Overview of Independent Churches and Charismatic Ministries in Ghana" in *Trinity Journal of Church and theology,*

Mzengi Manase E. "Lutheran Understanding of the Role of the Holy Spirit and Challenges from Pentecostal Churches in the ELCT Central Diocese." BD Thesis, Makumira University College, July 2003.

Truemper. David G."The Lutheran Confessional Writings and the Future of the Lutheran theology" in .*The Gift of Grace: The Future of the Lutheran theology.* Niels Henrik Gregersen, Bo Holm, et.al.Minneapolis:Fortress Press,1999.

Luther, *Katekismo Ndogo.TMW* - 688

Luther, *Augusburg Confession-Article XIII. In BC: 35*

*Tumwabudu Mungu wetu,*681

Luther. Martin. *Large Katechism. In The Book of Concord. The Confessions of the Lutheran Church, (*Theodore G. Tappert-Ed. (Philadelphia: Fortress Press,1959.

Luther. Martin. *BC Apology of the Augusburg Confession.*